TANGAZO LA SERIKALI NA. 927 la tarehe 15/11/2024

SHERIA YA MISITU,
(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 23)*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA HIFADHI YA MSITU WA MADABA WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MADABA YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Hifadhi ya Msitu wa Madaba wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

2. Eneo la ardhi lenye ukubwa wa hekta 662.93 au kilometa za mraba 6.23 zilizopo ndani ya ukomo na mipaka iliyoainishwa kwenye Jedwali la Notisi hii linapendekezwa kutangazwa kuwa Hifadhi ya Msitu wa Madaba wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba.

Madhumuni

3. Madhumuni ya kupendekeza kutangazwa Hifadhi ya Msitu wa Madaba wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba ni-

(a) kuhifadhi, kulinda na kutumia kwa uendelevu rasilimali za mazao ya misitu;
(b) kulinda na kuhifadhi baionuai na vyanzo vya maji vilivyo ndani ya msitu;
(c) kuwezesha uhifadhi na usimamizi wa eneo hilo; na
(d) kudhibiti matumizi ya rasilimali ya misitu.

*Tangazo la Serikali Na. 927 (Linaendelea)*

Sababu za kuwa msitu wa Halmashauri

4. Msitu unaopendekezwa kutangazwa utakuwa chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Madaba kwa lengo la kuongeza kipato cha Halmashauri kwa kupanda na kuvuna miti kwenye eneo lililotengwa kwa kuzingatia mpango, kuwajengea uwezo wananchi kwa ajili ya usimamizi mahiri wa msitu, kuhimiza mafunzo na utafiti katika msitu huo.

Uhalali wa Notisi

5. Notisi hii itakuwa halali kwa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa na ndani ya kipindi hicho mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza kwa maandishi-

(a) kupinga;
(b) kuwasilisha maoni; au
(c) kudai haki zozote zilizojikita kwenye na kutokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki zozote zilizojikita kwenye sheria nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kutangazwa Msitu wa Hifadhi Mumanga wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba.

Uwasilishaji wa pingamizi

6. Pingamizi lolote au maoni yoyote yatawasilishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa tisa na nusu mchana.

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Madaba,
S.L.P 10,
Madaba, Songea.

Muda na mahali kwa ajili ya mikutano au hadhara

7. Mikutano mikuu ya vijiji au mikutano ya hadhara kwa ajili ya kutoa ufafanuzi na kupokea maoni kuhusu pendekezo la kutangaza hifadhi husika itakuwa ikifanyika katika viwanja vya vijiji vya Ifinga na Wino kwa siku thelathini kutoka tarehe ya kutangazwa kwa Notisi hii kuanzia saa tatu asubuhi.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

HIFADHI YA MSITU WA MADABA WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MADABA

*Makadirio ya Eneo:* Hekta 662.93 au Kilometa za Mraba 6.23

Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la ardhi ya mataji wazi awali chini ya Msitu wa Madaba linalopatikana Wilaya ya Madaba, Mkoa wa Ruvuma kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Na. Jb 3130 ya Februari 2022 (Skeli 1:20,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, lenye mipaka ifuatayo:


| HIFADHI YA MSITU WA MADABA WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MADABA | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| *KIGINGI* | UELEKEO | UMBALI KATIKA META | MAJIRA NUKTA | | MAONI |
| NA. | | | *MASHARIKI* | *KASKAZINI* | |
| 1 | | | 767276 | 8932281 | |
| | Kalivinea | 234.96 | | | |
| 2 | | | 767070 | 8932168 | |
| | Kalivinea | 128.84 | | | |
| 3 | | | 767081 | 8932040 | |
| | Kalivinea | 245.84 | | | |
| 4 | | | 767232 | 8931846 | |
| | Kalivinea | 1024.90 | | | |
| 5 | | | 766208 | 8931803 | |
| | Kalivinea | 201.66 | | | |
| 6 | | | 766053 | 8931932 | |
| | Kalivinea | 559.30 | | | |
| 7 | | | 765545 | 8932166 | |
| | Kalivinea | 595.52 | | | |
| 8 | | | 765084 | 8932543 | |

*Tangazo la Serikali Na. 927 (Linaendelea)*

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kalivinea | 1073.71 | | | |
| 9 | | | 764183 | 8931959 | |
| | Kalivinea | 770.04 | | | |
| 10 | | | 763460 | 8931694 | |
| | Kalivinea | 885.69 | | | |
| 11 | | | 762575 | 8931729 | |
| | Kalivinea | 552.89 | | | |
| 12 | | | 762086 | 8931987 | |
| | 344$^{O}$34’ | 439.85 | | | |
| 13 | | | 761969 | 8932411 | |
| | 34$^{O}$36’ | 415.52 | | | |
| 14 | | | 762205 | 8932753 | |
| | 54$^{O}$26’ | 902.43 | | | |
| 15 | | | 762939 | 8933278 | |
| | 81$^{O}$5’ | 761.20 | | | |
| 16 | | | 763691 | 8933396 | |
| | 89$^{O}$13’ | 1239.12 | | | |
| 17 | | | 764930 | 8933413 | |
| | 99$^{O}$33’ | 801.12 | | | |
| 18 | | | 765720 | 8933280 | |
| | 131$^{O}$34’ | 577.33 | | | |
| 19 | | | 766152 | 8932897 | |
| | 146$^{O}$13’ | 480.09 | | | |
| 20 | | | 766419 | 8932498 | |
| | 104$^{O}$13’ | 884.05 | | | |
| 1 | | | 767276 | 8932281 | |

*Tangazo la Serikali Na. 927 (Linaendelea)*

**MADABA DISTRICT COUNCIL FOREST RESERVE**
**MADABA DISTRICT**
**AREA 622.93Ha OR 6.23SQ. KILOMETRS**




SCHEDULE

| BEACON NO | TRUE BEARING | DISTANCE IN METRES | CO-ORDINATES EASTINGS | NORTHINGS |
|---|---|---|---|---|
| MDC1 | | | 767276 | 8932281 |
| | Curvelinear | 234.96 | | |
| MDC2 | | | 767070 | 8932168 |
| | Curvelinear | 128.47 | | |
| MDC3 | | | 767081 | 8932040 |
| | Curvelinear | 245.84 | | |
| MDC4 | | | 767232 | 8931846 |
| | Curvelinear | 1024.90 | | |
| MDC5 | | | 766208 | 8931803 |
| | Curvelinear | 201.66 | | |
| MD2 | | | 766053 | 8931932 |
| | Curvelinear | 559.30 | | |
| MD3 | | | 765545 | 8932166 |
| | Curvelinear | 595.52 | | |
| MD4 | | | 765084 | 8932543 |
| | Curvelinear | 1073.71 | | |
| MD5 | | | 764183 | 8931959 |
| | Curvelinear | 770.04 | | |
| MD6 | | | 763460 | 8931694 |
| | Curvelinear | 885.69 | | |
| MD7 | | | 762575 | 8931729 |
| | Curvelinear | 552.89 | | |
| MD8 | | | 762086 | 8931987 |
| | 344°34' | 439.85 | | |
| KKKT1 | | | 761969 | 8932411 |
| | 34°36' | 415.52 | | |
| KKKT2 | | | 762206 | 8932753 |
| | 54°26' | 902.43 | | |
| KKKT3 | | | 762939 | 8933278 |
| | 81°5' | 761.20 | | |
| DK11 | | | 763691 | 8933396 |
| | 89°13' | 1239.12 | | |
| DK10 | | | 764930 | 8933413 |
| | 99°33' | 801.12 | | |
| DK9 | | | 765720 | 8933280 |
| | 131°34' | 577.33 | | |
| DK8 | | | 766152 | 8932897 |
| | 146°13' | 480.09 | | |
| DK7 | | | 766419 | 8932498 |
| | 104°13' | 884.05 | | |
| MDC1 | | | 767276 | 8932281 |

Dodoma,
30 Oktoba, 2024

PINDI HAZARA CHANA
*Waziri wa Maliasili na Utalii*